**Isichapishe kabla ya**: saa 04:00 asubuhi saa za Marekani / saa 8:00 mchana saa za GMT / saa 09:00 mchana Majira ya joto Uingrreza /saa 10:00 jioni saa kuu ya Ulaya

# Karne ya Uwekezaji katika Nishati Jadidifu, Nishati ya Jua Ikiongoza kwa dola za Marekani Trilioni 2.5

- Karne ya Uwekezaji (2010-2019) inaimarisha uwezo wake wa kuzalisha nishati jadidifu mara nne zaidi [1] kutoka gigawati 414 hadi gigawati 1,650
- Kuna uwezekano kuwa nishati ya jua pekee imeongezeka zaidi ya mara 26 kuliko kiwango kilichoshuhudiwa mwaka wa 2009 — kutoka gigawati 25 na kufikia taktibami gigawati 663
- Kiwango cha uwekezaji katika mwaka wa 2018 kilifia dola za Marekani bilioni 272.9, ikiwa ni ongezeko mara tatu zaidi katika uzalishaji wa nishati ya visikuku.
- Nishati jadidifu ilizalisha asili mia 12.9 ya umeme duniani katika mwaka wa 2018, na kuepuka kukuzalisha hewa ya kaboniksidi kwa tani bilioni 2.

**Frankfurt/Nairobi, September 5, 2019** – Kiwango cha uwekezaji katika aina mpya ya nishati jadidifu kote ulimwenguni katika karne hii — 2010 hadi 2019 ikijumuishwa pamoja — ina karibia kufikia dola za Marekani triilioni 2.6, huku mifumo iliyowekwa yanishati ya jua ikiongoza kwa gigawati nyingi kuliko kuliko mifumo mingine ya uzalishaji, kwa mjibu wa takwimu mpya zilizochapishwa leo.

Kulingana na ripoti ya *Global Trends in Renewable Energy Investment 2019* , iliyotolewa kabla ya Mkutano Mkuu wa Kushughulikia Mazingira Duniani wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa, kuna uwezekano uwekezaji huu utaongeza uzalishaji wa nishati jadidifu mara nne zaidi (bila kujumuisha vizalishaji vikubwa vya nishati ya maji) kutoka gigawati 414 mwishoni mwa mwaka wa 2009 hadi gigawati 1,650 wakati karne moja itakapotimia mwishoni mwa mwaka huu.

Nishati ya jua inakadiria nusu— dola za Marekani trilioni 1.3 — ya jumla ya dola za Marekani trilioni 2.6 katika uwekezaji wa nishati jadidifu uliofanyika katika karne nzima. Nishati ya jua pekee itakuwa imeimarika kutoka gigawati 25 mwanzoni mwa mwaka wa 2010 na inatarajiwa kufikia gigawati 663 kufikia mwishoni mwa mwaka wa 2019 — ina uwezo wa kuzalisha umeme wote unaohitajika kila mwaka kwa matumizi ya nyumbani Marekani kwa takribani nyumba milioni moja[2].

Uzalishaji wa umeme kote duniani kutokana na nishati jadidifu ulifikia asili mia 12.9, mwaka wa 2018, ikiwa ni ongezeko kutoka asili mia 11.6 katika mwaka wa 2017. Hii ilipunguza uzalishaji wa hewa ya kaboniksidi mwaka uliopita tu kwa takribani tani bilioni 2—ina manufaa ikichukuliwa kuwa sekta ya nishati duniani ilizalisha tani bilioni 13.7 za hewa katika mwaka wa 2018.

---

[1] Nishati jadidifu yote inayorejelewa katika makala haya haijajumuisha mabwawa makubwa yanayozalisha umeme wa zaidi ya megawati 50.
[2] Marekani ilikuwa na nyumba takribani milioni 128 mwaka wa 2018 (http://bit.ly/2HnX24S)

Tukijumuisha mifumo yote ya uzalishaji (visikuku na zile zisizozalisha hewa ya ukaa), karne inanuia kuzalisha nishati gigawati 2,366 huku nishati ya jua ikishikilia nafasi ya kwanza (gigawati 638 ), nafasi ya pili ilishikiliwa na makaa ya mawe (gigawati 529), na nishati ya jua na gesi zikichukuwa nafasi ya tatu na ya nne (gigawati 487 na gigawati 438 mtawalia).

Ushindani wa kuwekeza katika ya nishati jadidifu uliongezeka mno kati ya wawekezazi katika karne hii. Ukadiriaji wa gharama za umeme (hali inayowezesha kulinganisha mifumo mbalimbali inayotumika sanasana kuzalisha umeme) zilipungua kwa asili mia 81 ya bei ya vizio vya nguvu za umeme zinazotokana na jua tangu mwaka wa 2009; bei ya nishati inayotokana na upepo katika maeneo ya bahari ilipungua kwa asili mia 46.

"Kuwekeza kwenye nishati jadidifu ni kuwekeza kwa manufaa ya siku zijazo, jinsi inavyodhibitishwa kutokana na kuimarika zaidi kwa matumizi ya nishati jadidifu katika karne iliyopita," alisema Inger Andersen, Katibu Mtendaji wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa.

"Hatuwezi ridhika na kutulia kwa sababu ya hali hii. Uzalishaji wa nguvu za umeme kote ulimwenguni umeimarika kwa takribani asili mia 10 katika kipindi hiki. Ni wazi kuwa tunapaswa kuongeza kasi ya kuwezesha watu kutumia nishati jadidifu iwapo tunataka kufikia malengo ya kimataifa ya tabia nchi na ya maendeleo."

**Mwaka wa 2018 unashuhudia ongezeko la zaidi ya dola robo ya trilioni kwa mara nyingine**

Ripoti, inayotolewa kila mwaka tangu mwaka wa 2007, iliendelea na utamaduni wake kuangazia takwimu za kila mwaka, huku uwekezaji katika nishati jadidifu kote ulimwenguni ukifikia dola za Marekani bilioni 272.9 katika mwaka wa 2018.

Ijapokuwa ilipungua kwa asili mia 12 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia, mwaka wa 2018 ulikuwa mwaka wa tisa mtawalia ambapo uwekezaji ulikuwa zaidi ya dola za Marekani bilioni 200 na mwaka wa tano mtawalia kufikia zaidi ya dola za Marekani bilioni 250. Ilikuwa takribani mara tatu zaidi ya uwekezaji wa jumla kwa nishati ya makaa ya mawe na ya gesi.

Takwimu za mwaka wa 2018 zilifikiwa licha ya kuendelea kudorora kwa miradi ya nishati ya jua na nishati ya upepo, na licha ya mabadiliko ya sera ya uwekezaji iliyoshuhudiwa Uchina katika kipindi cha pili chaa nusu ya mwaka huo.

Rekodi ya nishati jadididfu ya gigawati 167 iliwekwa mwaka wa 2018, ikiwa ni ongezeko kutoka gigawati 160 zilizoshuhudiwa katika mwaka wa 2017.

Jon Moore, Afisa Mkuu Mtendaji wa BloombergNEF (BNEF), kampuni ya utafiti inayotoa data na uchanganuzi wake ili kutumika kwa maandalizi ya ripoti ya Global Trends alisema: "Kupungua kwa kiwango kikubwa cha bei ya umeme unaotokana na nishati ya upepo na nishati ya jua katika miaka ya hivi karibuni kumebadili mielekeo ya waunda sera. Teknolojia hizi, ambazo mara nyingi zililizalisha kiwango kidogo cha hewa ya ukaa zilitengenezwa kwa urahisi. Sasa, katika nchi nyingi kote ulimwenguni, kuna uwezekano mkubwa kuwa upepo au jua inazalisha umeme kwa gharama za chini zaidi."

Ripoti hiyo pia inafuatilia uwekezaji usioweza kukadiriwa katika nishati jadidifu — fedha zinazotumiwa kwenye teknolojia na katika kampuni za wataalamu wa nishati. Uwekezaji wate wa aina hii uliamarika katika mwaka wa 2018. Ongezeko la asli mia 10 ya dola za Marekani bilioni 13.1 lilishuhudiwa na serikali na mashirika ya utafiti na maendeleo. Hisa zilizo na riba ya kudumu zilizotokana na makampuni katika masoko huru ziliimarika kwa asili mia 6 kwa dola za Marekani bilioni 6, na mtaji kutokana na miradi na kutoka kwa hisa zilizo na riba ya kudumu kutokana na uwekezaji wa kibinafsi ulifikia asili mia 35 kwa dola za Marekani bilioni 2.

Uwekezaji kwenye nishati jadidifu kwa jumla, ikijumuisha makundi haya na uwekezaji katika uzalishaji wa nishati, ulifikia dola za Marekani bilioni 288.3 katika mwaka wa 2018, ikipungua kwa asili mia 11 ikilinganishwa na rekodi iliyowekwa mwaka wa 2017 ya dola za Marekani bilioni 325.

“Kuna teknolojia za kutumia upepo, jua au nishati inayotokana na joto duniani. Teknojia hizi zina uzuri sawa au zaidi ya teknolojia zingine na hazichafui mazingira. Katika kipindi cha miaka 10 Ujerumani itazilisha theluthi mbili za umeme wake kotokana na nishati jadidifu. Tunadhibitisha kuwa nchi iliyoendelea, yenye viwanda vingi inaweza kukoma kutumia makaa ya mawe, wakati uo huo, ikakomesha kutumia nishati ya nyuklia bila kuhatarisha uchumi wake,” alisema Svenja Schulze, Waziri wa Ujerumani wa Mazingira, Uhifadhi wa Mazingira na Usalama wa Nyuklia.

“Tunafahamu kuwa nishati jadidifu ina manufaa kwa hali ya hewa na kwa uchumi. Lakini hatujawekeza vya kutosha kuhakikisha hatuzalishi hewa ya ukaa tunapotumia umeme, vyombo vya usafiri na tunapopika ili kupunguza joto duniani hadi Selsha 2 au zinazokubalika za 1.5. Iwapo tuna maono ya kuwa na siku za usoni zilizo salama na endelevu tunapaswa kuongeza juhudi sasa kwa kutunga sheria zinazopendelea mazingira na kuweka miundo mbinu inayopendelea uwekezaji katika nishati jadidifu.

"Ni muhimu kuona kuwa nishati jadidifu inakuwa chaguo la kwanza katika maeneo mengi, alisema Nils Stieglitz, Rais wa kituo cha Frankfurt School of Finance and Management. "Lakini sasa tunapaswa kufikiria zaidi ya koboresha nishati jadidifu. Kuepuka kutumia makaa ya ni mojawapo tu ya masuala katika sekta pana ha Ufadhili wa Kudumu.Wawekezaji watajali zaidi iwapo upunguzaji wa hewa ya ukaa itakuwa na manufaa ya kudumu.”

**Uchina bado inaongoza, lakini uwekezaji katika nishati jadidifu umetamba kote**

Uchina imekuwa mwekezaji mkubwa zaidi katika uzalishaji wa nishati jadidifu katika karne hii, kwa


kuwekeza dola za Marekani bilioni 758 kati ya mwaka wa 2010 na nusu ya kwanza ya mwaka wa 2019, Marekani ikichukua nafasi ya pili kwa dola za Marekani bilioni 356 na Uerumani ikichukua nafasi ya tatu kwa dola za Marekani bilioni 202.

Ulaya kwa jumla iliwekeza dola za Marekani bilioni 698 katika uzalishaji wa nishati jadidifu katika kipindi hicho, huku Ujerumani ikichangia zaidi kwa dola za Marekani bilioni 179, na Uingereza kwa dola za Marekani bilioni 122.

Ijapokuwa Uchina ndiye mwekezaji wa pekee kuwekeza zaidi katika mwaka wa 2018 (kwa dola za Marekani bilioni 88.5, ikipungua kwa asili mia 38), uwekezaji katika uzalishaji wa nishati jadidifu ulidhihirika zaidi kote ulimwenguni mwaka jana, huku kila mojawapo wa nchi 29 zikiwekeza zaidi ya dola za Marekani bilioni 1, ikiwa ni ongezeko kutoka asili mia 25 katika mwaka wa 2017 na asili mia 21 katika mwaka wa 2016.

Ripoti ya *Global Trends in Renewable Energy Investment* huidhinishwa na Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa kwa ushirikiano wa Kituo cha Frankfurt School-UNEP Collaborating Centre for Climate & Sustainable Energy Finance na kutolewa kwa ushirikiano na BloombergNEF. Ripoti hii hudhaminiwa na Wizara ya Mazingira, Uhifadhi wa Mazingira, na Usalama wa Nyuklia nchini Ujerumani.

Figure 1: Uwekekezaji katika nishati jadidifu kwa kuzingatia nchi, kutoka mwaka wa 2010 hadi nusu ya kwanza ya mwaka wa 2019, kwa dola za Marekani.



Chanzo Global Trends in Renewable Energy Investment 2019, kwa kuzingatia data kutoka kwa BloombergNEF

Ripoti kamili, *Global Trends in Renewable Energy Investment 2019*, inaweza kutolewa kwa vyombo vya habari

Waandishi wa ripoti hii wanapatikana iwapo mahojiano yanahitajika kabla ya ripoti kutolewa. Pia watashiriki katika mahojiano na vyombo vya habari kwa njia ya simu Alhamisi tarehe 5, Septemba 2019, saa 2:00 asubuhi saa za Marekani / saa 6:00 mchana saa ya GMT /saa 7:00 mchana saa ya BST/ saa 8:00 mchana saa kuu ya Ulaya. kushiriki mahojiano ya simu bonyeza +1.408.740.7256, conf. ID: 4168788712, au bofya hapa: https://bluejeans.com/4168788712/browser

*Kwa maelezo zaidi:*


- Sophie Loran, UN Mazingira, + 33 1 44 37 42 73, sophie.loran@un.org
- Robert Leonardt, Frankfurt School of Finance & Management, +49 69 154008 818, r.leonardt@fs.de
- Veronika Henze, BloombergNEF, +1 646 324 1596, vhenze@bloomberg.net
- Terry Collins, +1-416-878-8712, tc@tca.tc
- Moses Osani, UN Mazingira, +254716145616, moses.osani@un.org